epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Mei 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581663
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital


HOTUBA Jumatano Mei 1, 2024 Nipashe 11

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAZIRI WA MADINI

HOTUBA YA MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb.)
Waziri wa Madini

Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.)
Naibu Waziri wa Madini

Bw. Kheri Abdul Mahimbali
Katibu Mkuu

Bw. Msafiri Lameck Mbibo
Naibu Katibu Mkuu

## HOTUBA YA WAZIRI WA MADINI, MH. ANTHONY MAVUNDE

UK. 11

**Serikali** na mkakati wa kuimarisha sekta ya madini nchini




UKURASA 3

**Utafiti** wafanywa athari za mikaratusi katika mazingira



UKURASA 5



**Bilioni 1/-** kuchangwa matibabu ya moyo watoto

UKURASA 5

## Wabunge wataka utafiti kuinusuru Shule ya Sheria

UKURASA 2



### MEI MOSI

# Matarajio nyongeza mshahara, kikokotoo

UKURASA 2&4



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Tundu Lissu (wa pili kulia), akiongoza maandamano ya wanachama na wafuasi wa chama hicho, jijini Dodoma jana, wakiishinikiza serikali kupatikana kwa katiba mpya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mil. 556/- kusaidia waathirika mafuriko

• **Bonite** yawakumbuka wa Kilimanjaro... *Endelea ukurasa 3*

**MICHEZO** **YANGA YACHAFUA TENA FAILI LAKE FIFA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Mkuu wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC), Balozi Meja Jenerali Wilbert Ibuge, wakati akizungumza alipofika na ujumbe wake, Ikulu jijini Zanzibar jana kwa ajili ya mazungumzo. **PICHA: IKULU**

# Matarajio mshahara, kikokotoo Mei Mosi

**Na Romana Mallya**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limesema matarajio ya wafanyakazi leo ni nyongeza ya mshahara ambao wanaamini ukiboreshwa vizuri mfanyakazi anapostaafu atapata mafao mazuri.

Kikubwa pia kinachosubiriwa ni kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kanuni mpya ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu.

Hivi karibuni, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, akijibu hoja mbalimbali za wabunge zilizoibuka bungeni, alisema suala la kanuni mpya ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu litajulikana Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi).

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana kwa njia ya simu kuhusu matarajio ya wafanyakazi leo, Makamu wa Rais wa TUCTA, Shabani Ambindwile, alisema matarajio yao ni kusikia nyongeza ya mshahara ambayo wanaamini mfanyakazi akipata mzuri atapata mafao mazuri.

"Mfanyakazi akitengenezewa mshahara vizuri atapata mafao mazuri. Upandishaji madaraja ni jambo ambalo serikali hufanya kila mwaka. Suala la kikokotoo lina taratibu zake," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi (TUGHE), Hery Mkunda, alisema wana matarajio mengi kutoka serikalini na wao wanaahidi kuendelea kushirikiana nayo.

Wakizungumza jana kwa sharti la kutotajwa majina baadhi ya wafanyakazi walisema, jambo kubwa wanalotaka kusikia ni nyongeza ya mshahara na suala la kikokotoo.

"Tunaamini Rais Samia atasikia kilio cha wafanyakazi. Tangu aingie madarakani tumeona mabadiliko kupitia uongozi wake, tunaamini atatufurahisha kesho (leo) Mei Mosi. "Mambo mengine tunayotarajia kusikia ni suala la upandishaji wa madaraja na ajira mpya ambayo inalenga kundi kubwa la vijana waliomaliza ngazi mbalimbali za elimu ikiwamo vyuo vikuu mbalimbali," alisema.

Katika majibu yake bungeni, Katambi alisema serikali haiwezi kufumbia macho wala masikio suala la kikokotoo.

Akifafanua kauli yake kuwa, "Rais amaishatoa maelekezo zaidi ya mara mbili, kwamba tulifanyie mapitio upya kuona namna ya kukifanyia maboresho zaidi ili wastaafu wasipate shida, tayari tumeanza kazi hiyo na sheria inatutaka kufanyia maboresho kila baada ya miaka mitatu na tayari imepita.

...Tunaendelea kulifanyia kazi maana tumepokea maelekezo ya Rais pamoja na Bunge, lakini pengine tunaweza kusikia kauli ya Rais katika viwanja vya Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, siku ya Mei Mosi atakapokutana na wafanyakazi kueleza suala hili, hivyo tumelipa uzito unaostahili kuhakikisha tunaliweka sawa," aliahidi.

Siku ya wafanyakazi hutumika kama sehemu ya kuwasilisha changamoto za wafanyakazi kwa mwajiri ili zipatiwe ufumbuzi.

Kilio kikubwa hasa kwa watu wanaostaafu kufanyakazi ni kikokotoo ambacho kinadaiwa hakiendani na muda waliotumia kufanyakazi.

Suala hilo pia limewaibua wabunge katika mijadala inayoendelea bungeni, mawaziri wanapowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara zao.

Mbunge ambaye mara kwa mara husimama bungeni kulipambania ni Esther Bulaya (CHADEMA), ambaye anapinga kikokotoo cha asilimia 33 akitaka kirudishwe cha asilimia 50 ili wastaafu waweze kuishi maisha yasiyokuwa na mawazo.

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, NSSF na PSSSF ndio yenye dhamana ya kuhifadhi michango ya wafanyakazi kwa kuifanyia miradi ya uzalishaji ya kuwanufaisha wanachama wake.

## Wabunge wataka utafiti kuinusuru Shule ya Sheria

**Na Vitus Audax,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kufanya utafiti wa kina kuhusu idadi kubwa ya wanafunzi wa Shule ya Sheria Tanzania (LST) kushindwa mitihani na kubaini mzizi wa tatizo hilo na kuja na suluhisho la kudumu ikiwa ni pamoja na kuweka mchujo wa wanafunzi kabla ya kuanza masomo hayo.

Mbunge wa Jimbo la Manyoni (CCM), Dk. Pius Chaya, alisema hali ya kufeli kwa wanafunzi wanaosoma shule ya sheria nchini imekuwa ya mwendelezo kila mwaka na kuonesha upungufu katika maeneo mbalimbali yanayotakiwa kufanyiwa kazi ili kurejesha heshima yake.

Alitaja upungufu huo kuwa ni pamoja na utofauti wa vyuo vinavyotoa shahada ya sheria nchini kutokana na uwekezaji pamoja na utofauti katika ufundishaji hali inayosababisha baadhi ya wahitimu wa vyuo fulani kufaulu mitihani hiyo huku wengine wakishindwa.

Aidha, alishauri serikali kuwaka mchujo kwa wanafunzi wanaotoka vyuoni kwa kufanya mtihani utakaowaruhusu kuendelea na masomo huku watakaoshindwa mtihani huo waendelee na shughuli nyingine zinazohusiana na taaluma hiyo kuliko kuendelea kupoteza muda wao.

Dk. Chaya alitoa mapendekezo kuwa serikali ije na mkakati wa kubadilisha mtaala wake ili uegemee zaidi katika utolewaji wa elimu kwa vitendo zaidi ya kusoma kama walivyokuwa wakisoma vyuoni.

Alisema haja ya serikali kutumia wataalamu waliobobea katika masuala ya sheria kwa vitendo kuliko wale waliobobea kwenye taaluma ya ufundishaji pekee kwani shule hiyo ipo kwa ajili ya kufundisha sheria kwa vitendo zaidi.

Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba, alisema wanafunzi wanaoingia katika shule ya sheria wanakuwa na ufaulu wa juu, lakini cha kushangaza wanaofaulu ni wachache.

Alisema wapo wanaosoma katika shule hiyo na kufeli masomo yao kisha kuachana na masomo hayo na kuendelea na shahada ya uzamili na kupata ufaulu wa juu kwa masomo hayo hayo.

"Naomba kwenye suala hili tusifanye utafiti wa kisiasa bali tufanye utafiti wa kitaalamu kwa sababu hakuna 'kilaza' (mjinga) anayesoma sheria kwenye nchi hii kwani kila anayesoma sheria ni yule aliyepata wastani wa juu kuanzia kidato cha nne hadi chuo kikuu," alisisitiza Salome.

Akijibu hoja hizo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, alisema tayari mapitio ya mtaala yameanza kufanyika na kuwa mtaala mpya utaanza kutumika ifikapo Julai 2024.

Dk. Chana alisema shule hiyo ya sheria imewekwa kwa mujibu wa sheria na kuwa kila mwanafunzi anayeanza masomo hapo lazima awe amekidhi vigezo ikiwa ni pamoja na kuwa na shahada ya sheria (LLB) hiyo kigezo hicho kinatosha kuendelea na masomo bila kuwekewa mtihani wa kuchujwa.

"Law School of Tanzania imekuwa ikiwatumia wataalamu wabobezi na kwa sasa ina kanzi data yenye wabobezi zaidi ya 80 kutoka kwenye maeneo mbalimbali ya kisheria wakiwamo majaji, mawakili wa serikali na mawakili wa kijitegemea hivyo mapendekezo mengine yaliyotolewa yataendelea kufanyiwa kazi," alisema Dk. Chana.

# Macho na masikio yanapoisubiri serikali hatima kikokotoo chao




**Na Gaudensia Mngumi**

NI siku ya wafanyakazi duniani, ambayo kama kawaida malalamiko mwaka huu ni kikokotoo 'umiza' cha mafao kiduchu ya pensheni kwa uwiano wa 33:67, ambao mstaafu analipwa asilimia 33 na kiasi kingine kinabakia hazina.

Kilio cha wafanyakazi ni kikubwa, mbali na mafao kuwa kidogo, yana masharti mfano ukifariki siku chache baada ya kuanza kulipwa pensheni, licha ya kuacha asilimia 67 ya fedha zake hazina, warithi watalipwa kwa miaka mitatu pekee.

Katibu Mkuu wa Chama cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu (CHAKAMWATA), Meshack Kapange, anakumbusha kuwa kilio ni kile kile mishahara midogo na hali ngumu.

Kapange, anasema hayo anapozungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam kuhusu maadhimisho ya sikukuu ya wafanyakazi na adha zinazowakabili.

Anasema mshahara wa mwalimu ni mdogo na katika sekta binafsi wanalipwa hadi Sh. 250,000 kwa mwezi bila kuchangia mifuko ya jamii wala bima ya afya licha ya kwamba shule hizo hutoza zaidi ya Sh. 2,000,000 kama ada kwa kila mwanafunzi.

"Lakini tumlaumu nani? Sera zote za uchumi, za kisiasa na maendeleo hazimhusishi mfanyakazi, zinapangwa na wanasiasa, wafanyabiashara na wawekezaji wa kigeni. Wakulima na wafanyakazi ambao ndilo kundi kubwa nchini, hakuna anayewahusisha kwenye kuandaa sera wala sheria licha ya kwamba zinagusa hatima ya maisha yao," anasema.

Anaongeza: "Nitoe mfano, sera ya Tanzania kwenye biashara, inapendelea anapoanza halipi kodi. Anajisikilizia haguswi na TRA lakini mfanyakazi wa Tanzania anapoajiriwa, akipata mshahara juu ya kima cha chini cha 270,000 anaanza kukatwa kodi ya mshahara (PAYE). Hii ikoje?" Anahoji.

> **TUCTA ina vyama vya wafanyakazi 14 pekee wakati kitaifa viko 34 na kwamba haijawa na nguvu ya kuwa sauti ya wafanyakazi wengi wanaohitaji kuwasilishiwa matatizo yao kwenye ngazi za uamuzi.**



Katibu Mkuu wa CHAKAMWATA, Meshack Kapange.

Akifafanua namna ambavyo kodi zinawaumiza wafanyakazi, Kapange anasema wanakatwa kodi hata kabla ya kupokea mshahara.

Anawageukia wafanyabiashara kuwa wanakadiriwa kodi wakati hali ni tofauti kwa wafanyakazi ambao wanakatwa hata kabla ya kupokea ujira wa mwezi.

"Wafanyabiashara na wawekezaji wanakadiriwa kodi za biashara zao. Wengine yanaamua cha kulipwa TRA. Ndio maana nasema wafanyakazi tuna kazi kubwa," anasema Kapange.

Kwa mujibu wa sheria za TRA, kiwango cha juu cha PAYE ni asilimia 30, hata hivyo mfanyakazi anayepokea kima cha chini cha mshahara ambacho ni Shilingi 270,000 halipi kodi ya mshahara. PAYE inakatwa na waajiri kabla wafanyakazi hawajapokea mishahara ni moja ya chanzo cha uhakika cha mapato ya serikali.

**TUMEBAKI YATIMA**

Katibu wa CHAKAMWATA anasema wafanyakazi hawana mtu wa kuwatetea akitoa mfano kilio cha kikotoo kinachoumiza kinazungumzwa na wabunge na kwenye maandamano ya CHADEMA kuna bango linalosomeka 'kikokotoo kiondolewe'.

Anahoji jukumu muhimu la Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi katika kutatua kiza hicho kinachowaumiza wataafu.

Anasema TUCTA ina vyama vya wafanyakazi 14 pekee wakati kitaifa viko 34 na kwamba haijawa na nguvu ya kuwa sauti ya wafanyakazi wengi wanaohitaji kuwasilishiwa matatizo yao kwenye ngazi za uamuzi.

"Ukifanya mahesabu utagundua kwamba mfanyakazi wa Tanzania analipwa siku 12 tu katika mwezi mzima anaofanyakazi, ndio maana kilio chao kila siku hawana kitu mfukoni, hali ni ngumu, njaa kali na madeni yasiyoisha," anasema.

Anatoa mfano wa mikopo ya kausha damu au umiza ambayo imewaathiri zaidi wafanyakazi hasa kada ya ualimu ambao baadhi wamepoteza maisha, mali, msongo wa mawazo, kuvuruga familia na uhusiano wa kijamii.

**MIKOPO UMIZA**

Kapange akifafanua zaidi anasema mikopo kausha damu imesababisha uhasama kazini kutokana na wadhamini na watu wa karibu kulazimika kulipa madeni ya mikopo hiyo hatarishi.

"Walimu, ndugu wa karibu, viongozi wa serikali za mitaa na vijiji wote wameingizwa kwenye migogoro baada ya waliokopa kushindwa kulipa madeni. Ni jambo linalohitaji kufanyiwa utafiti na bila shaka mojawapo ya chanzo kikubwa cha shida yote hii ni mishahara duni na mafao yasiyo ya uhakika," anasema Kapange.

Anaeleza kuwa Tanzania ni nchi ambayo mfanyakazi anapata pensheni baada ya kuchangia kwenye mfuko kwa miaka 15 wakati hali ni tofauti huko Rwanda, wafanyakazi wanasifa ya kulipwa mafao baada ya kuchangia kwa miaka saba.

Anasema pamoja na sharti hilo, kwa Tanzania mafao na mishahara ni midogo, jambo ambalo linawafanya wafanyakazi wengi kuishi kinyonge, kimaskini kutokana na kwamba hawawezi kumudu milo mitatu wala maji anayohitaji kutumia kwa siku.

"Cha kusikitisha ni kwamba hakuna dalili ya kuwa na taasisi inayosimama kidete kutafuta namna ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizi," anasema Kapange.

Hata hivyo, mtaalamu wa uchumi Dk. Hoseana Lunogelo, anasema suala la maslahi bora ya wafanyakazi linapatikana iwapo kutakuwa na fursa nyingi za ajira kama viwanda na uwekezaji unaochochea uzalishaji wa bidhaa na huduma.

Anashauri wafanyakazi kufikiria kuanzisha viwanda ili nao waongeze nafasi za ajira, tija na kuzalisha bidhaa na huduma bora zaidi kutoka zilizopo.

Anatoa mfano wa kinu cha chambua pamba kwenye mikoa ya kanda ya ziwa ambacho kwa miaka mingi kinachambua na kuuza nyuzi za pamba pekee bila kuongeza thamani na kwamba kuna fursa ya kuanzisha kiwanda cha nguo za aina mbalimbali.

"Kwa kuendelea kuuza bidhaa zisizoongezewa thamani, mshahara wala mapato ya mfanyakazi haviwezi kuongezeka. Kadhalika, watu wanauza asali lakini ingesindikwa ikazalisha dawa kwa mfano au bidhaa nyinginezo, ingeongeza ajira na mshahara pia," anasema.

"Tuondoke kwenye 'comfort zone' huu umazoea, kufikiria nyongeza ya mishahara kila Mei Mosi na kuajiriwa, tubadilishe mitazamo na tuanzishe viwanda na kuwa na ubunifu na utafiti wa kuongeza mapato na ajira kwa wengine," anafafanua, mtaalamu huyo.

## Mbowe atoa tathmini ya maandamano kwa mikoa 13

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

WAKATI Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kikihitimisha jana awamu ya kwanza ya maandamano yake katika mikoa 13 nchini, Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe, ametoa tathmini ya maandamano hayo kwamba yalilenga mambo manne.

Miongoni mwa mambo hayo ni kueleza Watanzania namna Tume Huru ya Uchaguzi iliyoundwa kisheria hivi karibuni ilivyo na matobo.

Akihutubia mamia ya wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro katika Uwanja wa Mashujaa, mjini hapa, Mbowe alisema mfumo wa uchaguzi kama ulivyo sasa nchini una matobo na unatoa upendeleo wa makusudi kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kushinda bila ridhaa ya wananchi.

"Maandamano ya awamu ya kwanza ya mikoa ambayo tunahitimisha leo (jana) Moshi, yalikuwa na malengo manne ambayo ni kushinikiza kupata katiba mpya na katiba bora itakayotibu maumivu, uonevu, utawanyaji wa rasilimali za nchi na itakayoleta utawala bora na kuhakikisha maisha bora kwa kila Mtanzania.

"Tuliamini tunapaswa kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, ambayo itasababisha kupatikana kwa viongozi wenye hofu ya Mungu wanaopatikana katika chaguzi huru na chaguzi za haki. Lakini mfumo wetu wa uchaguzi kama ulivyo leo, ni mfumo wenye matobo ambao unatoa upendeleo wa makusudi kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kushinda bila ridhaa ya wananchi," alisema huku akibainisha katika mikoa hiyo ametembea kilomita 111.

"Tumeanza maandamano Aprili 22 nimetembea kilomita za kutosha. Tunapohitimisha hapa (Moshi) Makamu Mwenyekiti Bara, Tundu Lissu, yuko Morogoro anahitimisha. Tunaanza tena awamu ya pili katika mikoa yote iliyobakia na kama hawasikii tukimaliza tunaanza kwenye wilaya," aliongeza.

Mpaka sasa awamu ya kwanza ya maandamano ya ngazi ya mikoa, CHADEMA imefanya katika mikoa ya Kagera, Mara, Geita, Mwanza, Shinyanga, Katavi, Simiyu, Dodoma, Morogoro, Singida, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA, Benson Kigaila, alitaja chanzo cha matatizo yote hayo ni ya ugumu wa maisha, ni utawala wa CCM na kuwataka kuunganisha nguvu pamoja na kuleta mabadiliko.

"Maisha ni magumu, vitu vimepanda bei mwananchi wa hali ya chini anateseka, hii yote ni kutokana na kukosekana kwa utawala bora wa Chama Cha Mapinduzi(CCM).Tujiunge na CHADEMA tuiuwe CCM katika chaguzi za serikali za mitaa mwaka 2024 na matanga yao yawe 2025 katika serikali kuu," alisema Kigaila.

Mbunge wa zamani wa Moshi Mjini, Jafary Michael, aliwataka wananchi kujitokeza kujitetea katika kujiletea maendeleo na kuleta mabadiliko chanya kwa taifa.

Aidha, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, Grace Kiwelu, aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi katika chaguzi za serikali za mitaa ili kuondoa mapandikizi ya CCM yaliyowekwa na hayati John Pombe Magufuli.

"Tukimaliza uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 twendeni kwenye uchaguzi mkuu 2025 na kuhakikisha tunaleta mabadiliko na kukomboa majimbo yote yaliyochukuliwa CCM," alisema Kiwelu.

Awali, Mwenyekiti wa CHADEMA Moshi Mjini, Raymond Mboya, alisema tangu Manispaa ya Moshi kuchukuliwa na CCM, masoko yameungua zaidi ya mara tatu.

"Wananchi wamepoteza mikopo na serikali ilitoa mwezi mmoja ili kujenga soko, lakini hadi sasa miezi mitatu soko hilo halijajengwa, zipo taarifa kuwa wapo vigogo wa manispaa ya Moshi wanashindana ili kupata tenda na hii ndiyo inayochelewesha ujengaji wa soko hilo.

# Bilioni 1/- kuchangishwa matibabu moyo watoto

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na Heart Team Africa Foundation (HTAF), imeandaa hafla ya kuchangisha Shilingi bilioni moja kwa ajili ya matibabu ya watoto.

Fedha hizo zinatarajiwa kukusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali katika hafla itakayofanyika Julai 6, mwaka huu, wakati wa chakula cha hisani zitafanikisha upasuaji wa moyo kwa watoto 500.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kubainisha kuwa hatua hiyo inaunga mkono jitihada za serikali kuwatibu watoto wanaougua magonjwa ya moyo.

"Asilimia 70 ya gharama za matibabu kwa watoto huchangiwa na serikali. Pamoja na kuchangiwa, bado asilimia 80 hawamudu gharama hizo kwa asilimia 30 iliyobaki. Kiwango cha gharama kwa upasuaji kwa mtoto mmoja ni kati ya Sh. milioni nne hadi 15.

"Kwa mwaka, JKCI inafanya upasuaji kwa watoto 357. Kwa harambee hii tutaongeza upasuaji watoto kutoka idadi hiyo hadi watoto 500," alisema Dk. Kisenge.

Alisema ushirikiano kati ya JKCI na HTAF ulianza mwaka jana kwa nia ya kusaidia watoto wenye magonjwa ya moyo na kuungana na serikali katika kusaidia matibabu ya watoto.

"Watoto wengi wanapata tatizo la moyo kwa kuzaliwa nalo na katika watoto 100 mmoja ana tatizo la moyo. Pia inakadiriwa nchini kwa wastani wa watoto milioni mbili wanaozaliwa kwa mwaka nchini, 13,000 hadi 14,000 kati yao wana tatizo hilo na 4,000 watahitaji upasuaji wa moyo," aliongeza.

Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Moyo na Bingwa wa Magonjwa ya Moyo JKCI, Dk. Sulende Kubhoja, alisema ongezeko la idadi ya watu nchini, linakwenda sambamba na idadi ya watoto wanaozaliwa na matatizo ya moyo.

"Mwaka 1962 Watanzania tulikuwa takribani milioni 10 na sasa ni milioni 61. Asilimia 60 nchini ni watoto walio na umri wa miaka 16. Asilimia 80 ya Watanzania ni walio katika umri wa miaka 40 ambao wako kwenye umri wa kuzaa.

"Kwa wastani watoto milioni mbili huzaliwa kila mwaka na katika hawa, kuna watoto takribani 10,000 wanazaliwa na tatizo la moyo na wengine watahitaji upasuaji. Upasuaji mmoja unaweza kufika Sh. milioni 15 hadi 20," alisema bingwa huyo.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa HTAF, Linda Gideon, alisema lengo la kuandaa harambee hiyo ni kusaidia familia ambazo watoto wao wanaugua magonjwa ya moyo na kuhitaji upasuaji, huku hali zao zikiwa duni kifedha.

"Kwa mwaka huu taasisi inatarajia kukusanya fedha na kuwafanyia upasuaji watoto 200. Tunaomba wadau tofauti kutuunga mkono kwa kuchangia," alisema.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, Seleman Maulid, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Imalilo, wilayani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafanya utafiti athari za mikaratusi katika mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) inaendelea na utafiti wa kina wa miti aina ya mikaratusi kuhusu athari zake kimazingira na kuja na taarifa ya kitaalamu pamoja na ushauri, Bunge lilielezwa jana mjini hapa.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Khamis, alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe.

Katika swali hilo, Mafuwe alitaka kujua tamko la serikali kuhusu kuteketeza miti ya mikaratusi nchini baada ya utafiti kuonyesha kuwa inaharibu mazingira.

Akijibu swali hilo, Khamis alisema baada ya utafiti kukamilika, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii zitatoa elimu kwa wananchi kuhusu miti hiyo.

Alisema kuna zaidi ya aina 500 za miti ya mikaratusi duniani na Tanzania kupitia TAFORI, imeruhusu aina 25 za miti hiyo ili kupata fursa mbalimbali zitokanazo na mikaratusi hasa kwenye viwanda vya mazao yaliyosindikwa.

"Serikali kupitia Wizara ya Maji, Maliasili na Utalii pamoja na sisi Mazingira tumegundua iko miti inayokunywa maji na inapunguza au kuchangia vyanzo vya maji kupotea. Pia tumegundua ziko aina tofauti kwa mfano ziko zaidi ya 20 na zinatumia maji, hivyo tuko katika mpango wa kuzifanyia utafiti," alisema.

Hata hivyo, aliwahimiza wananchi kuendelea kupanda miti kwa wingi wakati serikali inaendelea kufanya tafiti kuhusu miti ya mikaratusi kubaini athari za kimazingira.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha wafanyakazi kuhusu kikokotoo kipatiwe ufumbuzi

**LEO** ni Siku ya Wafanyakazi Duniani, maarufu kama Mei Mosi. Wafanyakazi duniani kote wanasherehekea siku hii ikiwa ni sehemu ya kumbukumbu ya wenzao waliouawa miaka ya 1880 walipoandamana kudai haki na maslahi bora pamoja na saa za kufanya kazi.

Wafanyakazi hao walikuwa wakitaka saa za kufanya kazi zipunguzwe kutoka 12 hadi nane kwa siku pia kuwapo saa moja kati ya hizo kwa ajili ya mapumziko na chakula na malipo ya saa za ziada. Sambamba na hayo, walitaka pia kuwapo kwa likizo ya mwezi kila mwaka ili kumpa mfanyakazi muda wa kupumzika baada ya kufanya kazi takriban mwaka mzima.

Katika kuadhimisha sikukuu hii, wafanyakazi wa taasisi mbalimbali, za umma na za binafsi, hukusanyika katika maeneo mbalimbali huku wakionyesha bidhaa au shughuli wanazofanya huku wakiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali ambayo pamoja na mambo mengine, husisitiza tija na ufanisi mahali pa kazi, na maslahi bora.

Watanzania katika kuadhimisha siku hii ambayo kitaifa inafanyika Arusha, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni "Nyongeza ya Mishahara ni Msingi wa Mafao Bora na Kinga Dhidi ya Hali Ngumu ya Maisha".

Kaulimbiu hii inasadifu na hali ya sasa ya maisha ya wafanyakazi wengi, hasa serikalini, ambao kilio chao kikubwa ni kutoongezwa mishahara kwa miaka kadhaa pamoja na malalamiko ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu kwamba kinawaumiza wengi na kwamba hata baada ya kustaafu wanakuwa katika maisha magumu. Kutokana na hali hiyo, ni wazi kwamba serikali ambayo siku zote imekuwa ikisema ni sikivu, itatoa kauli kuhusu jambo hilo na kuwafanya wafanyakazi wengi kuwa na kicheko.

Suala la kikokotoo limepigiwa kelele tangu yalipofanyika mabadiliko mwaka 2018 kwamba mfanyakazi anapostaafu achukue malipo ya mkupuo asilimia 25 na kiasi kilichobaki achukue kidogo kidogo kwa muda wa miaka 12.5. Baada ya vuta nikuvute ya takriban mwaka, serikali chini ya aliyekuwa Rais John Magufuli, ilisimamisha hadi mwaka 2023 na kutaka majadiliano yafanyike ili kuwapo na maelewano baina ya wafanyakazi kupitia vyama vya wafanyakazi na serikali yenyewe.

Hatimaye mwaka jana yalifanyika tena mabadiliko na kuamuliwa kwamba malipo ya mkupuo yawe asilimia 33 kwa wafanyakazi wote wa serikali na sekta binafsi jambo ambalo limekuwa ikilalamikiwa pia kwamba kiwango hicho badi ni matesi kwa mtumishi. Swali linalokuja ni kwamba iweje mfanyakazi huyo ambaye ametumika kwa uaminifu na kupoteza nguvu zake katika kazi ajira apewe kiasi kidogo huku kukiwa na msemo wenye mzaha kwamba akipewa kiasi kikubwa atatumia ovyo na hatimaye ataishiwa, hivyo kuwa kuishi kwa taabu katika miaka iliyobaki.

Ili kufikia mwafaka, kwa mujibu wa Rais wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, kikokotoo kibadilishwe na kutoka asilimia 33 ya sasa hadi 50 kwa malipo ya mkupuo na kanuni ya ukokotoaji iwe 1/540 kama ilivyokuwa zamani badala ya 1/580 ya sasa.

Jambo hilo pia limezungumzwa kwa kina na baadhi ya wabunge na viongozi wa vyama vya siasa kwamba mfanyakazi huyo ambaye amefanya kazi kwa nguvu zote na hatimaye kufikia umri wa kustaafu, ni vyema apewe stahili yake ili afurahie jasho lake alilolitoa katika utumishi badala ya kubanwa na kukejeliwa kwamba hana uwezo wa kutunza fedha zake, hivyo apewe kiasi na kinachobaki atachukua kidogo kidogo.

Aidha, katika mfumo huo wa mafao, inabainishwa kwamba iwapo mfanyakazi huyo atafariki kabla ya miaka 12.5 ya kuchukua kidogo kidogo, basi wategemezi wake watapokea mafao hayo kwa miaka mitatu pekee!

Katika suala hili, ni vyema kukafikiwa mwafaka kama Rais Samia anavyotaka mambo yaendeshwe kwa 4R ikiwamo 'Reconciliation' (maridhiano) ambayo ni msingi bora katika kukubaliana kwenye jambo lolote badala ya kuacha upande mmoja ukinung'unika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanawake wana haki ya ajira bora

Na Gaudensia Mngumi

**FURAHA**, afya ya akili na mwili ukiwa nyumbani na kazini inawawezesha watu kuishi maisha yenye tija kiuchumi na kijamii.

Wakati huu wa kusherehekea na kutafakari dunia ya kazi, na mafanikio ya kutumia nguvukazi kwenye sekta ya kazi, tunajiuliza wanawake wana furaha na afya ya akili na kimwili kazini?

Ndipo linapokuja suala la kuugeukia upya mjadala wa kuwa na usawa wa kijinsia kazini, sera na miongono ya kupunguza ukandamizaji wa wanawake sehemu za kazi.

Dhana ya rasilimali watu au mtaji wa binadamu inawachukulia wanadamu kama vyombo au zana za kiuchumi zinazozalisha na kubadilisha maisha ili kupata hali bora zaidi kupitia nguvu za misuli na akili.

Lakini licha ya wanawake kuwa sehemu ya nguvukazi bado hali halisi ya utumishi wao kazini kwa kiasi kikubwa inawaona kama hawaajiriki na wanawekwa nyuma kwenye masuala ya ajira rasmi.

Watetezi wa maendeleo na haki za wanawake wanaona kuwa rushwa ya ngono, mishahara kidogo, kutoaminiwa na kupewa nafasi za uongozi bado ni tatizo linalowakabili wanawake wengi sehemu za kazi.

Kwa ujumla ajira kwa wanawake si rahisi kama ilivyo kwa wanaume. Waajiri wanawakwepa kisa, kuhofia uzazi na likizo za mateniti ambazo pia wanatakiwa kuwalipa watumishi hao wazazi.

Wanawachukulia wanawake kuwa ni mzigo hasa wakati wa ujauzito. Muda mwingine ujauzito ni tiketi ya kufukuzwa kazi. Kisingizio ni kwamba nafasi ya kazi yako imechukuliwa na mwingine.

Wanakwepa pia kuwaajiri kwa kuhofia kuwapa ruhusa za kupumzika wakati huo, kwenda kuwatibu watoto na kuhudumia wanapokuwa wagonjwa, wakihusisha shida hizo na upotevu wa mapato.

Mbali na hali hiyo kuwanyima wanawake fursa za ajira rasmi, wengi wakibakia vibarua kadhalika kundi hili ni wahanga wa unyanyasaji kingono.

Wapo viongozi, wakuu wa idara na watumishi wengine wanaowanyanyasa kingono kama kisingizio cha kuwapa kazi au kulinda ajira zao.

Ni lazima sasa msisitizo uwekwe sehemu za kazi kupinga unyanyasaji kijinsia na rushwa ya ngono. Lakini, kudumisha na kurejesha matumizi sahihi ya sheria za kazi ambazo zinawapa kinamama haki ya ajira.

Wenye viwanda na kampuni wafahamu kuwa hakuna nguvu kazi bila familia yaani uzazi, hivyo waajiri watimize mahitaji ya kazi kisheria ili kuondoa unyanyasaji kwa watumishi wanawake.

Kama inawezekana mahali pa kazi pawe na huduma zote muhimu na panapofuata sheria, sera, kanuni na taratibu bila kubagua kundi fulani.

Ikumbukwe kuna mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) wa wafanyakazi wenye majukumu ya familia namba 156 wa mwaka 1981 bado una nafasi.

Japo hadi sasa umeridhiwa na mataifa machache ikilinganishwa na wake walioridhia mkataba wa kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake, ambao umeridhiwa na mataifa yote.

Leo, inapoadhimishwa Mei Mosi uwekezaji katika wanawake na ajira ni muhimu ili kuwawezesha kuwa na mazingira bora kazini na maendeleo ili kupunguza pengo la umaskini baina ya wanawake na wanaume.

Ni karne ya 21, msichana au mfanyakazi wa kiwanda ni tofauti na mtumishi wa ndani, mwenye ajira anazalisha kiuchumi na anaweza kubadilisha maisha yake, hivyo ni wakati wa kuwaondoa wanawake kwenye kazi duni.

Itakumbukwa kuwa mwanasayansi Charles Darwin alikuja na kanuni ya "kuishi ni kuwa na msuli kwa walio na nguvu zaidi hao ndiyo watakaoishi".

Ni kanuni ya 'the survival of the fittest', ndicho kinachoweza kuonekana zama hizi kama wanawake hawatapewa nguvu kwenye kupata ajira, kufahamu teknolojia mpya ya kidijitali na ubunifu.Ni lazima kuzingatia mahitaji ya wafanyakazi wanawake na changamoto zinazokabili katika kuongeza uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa.

Maendeleo ya uchumi ni lazima yawe na usawa kuzuia kupotevu na kuharibu wa uwezo wa wanawake kwenye kuchangia uchumi wao binafsi na wa taifa pia.

## Vivuko Dar vyang'oa wawili TEMESA

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amewaondoa watendaji wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) katika nafasi zao kwa kushindwa kusimamia kikamilifu huduma bora kwa wananchi wanaotumia usafiri wa kivuko kati ya Magogoni-Kigamboni.

Waliondolewa ni Meneja wa Vivuko Kanda ya Mashariki na Kusini, Mhandisi Lukombe King'ombe na Mkuu wa Kivuko cha Magogoni -Kigamboni, Idd Stamili Juma, ambao watapangiwa kazi nyingine.

Waziri Bashungwa alitoa maagizo hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati akikagua huduma zinazotolewa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) na kusikiliza changamoto za wananchi wanaotumia usafiri wa vivuko kati ya Magogoni-Kigamboni na kuonyesha kutoridhishwa na utoaji wa huduma za wakala huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Ujenzi, Bashungwa amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Balozi Mhandisi Aisha Amour, kupeleka timu mpya.

Aliitaka timu hiyo mpya ikashirikiane kwa karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni ili kuhakikisha kuwa, wananchi wanapata huduma bora za vivuko katika maeneo hayo.

"Nikuagize Katibu Mkuu kuangalia namna ambavyo utawabadilishia mazingira na kuwapa majukumu mengine Meneja wa Kanda na Mkuu wa Kivuko cha Magogoni-Kigamboni na kuleta watendaji wapya ambao watamsaidia Mtendaji Mkuu wa TEMESA kusimamia mkakati mpya wa maboresho ya TEMESA," aliagiza.

Waziri Bashungwa pia, alimwelekeza Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kilahala, kuanza mara moja kufanya maboresho katika majengo ya abiria katika maeneo yote nchini yenye huduma za vivuko, ambapo ameelekeza kuanza kuondoa feni mbovu na kuweka mpya katika eneo la Magogoni-Kigamboni.

"Nimekagua na nimejionea mwenyewe sehemu ya jengo la abiria linahitaji maboresho na usafi, nimeona zile feni kwanza ikiwashwa unakimbia kwa lile vumbi lililoko unaweza ukapata madhara makubwa ya kiafya, hivyo zile feni ziondolewe mara moja.

"Nimechukizwa na majibu yaliyokuwa yakitolewa. Sidhani kama wizara kupitia TEMESA tunaweza kushindwa mambo madogo madogo kama haya," alisema.

Kuhusu changamoto za mfumo wa malipo wa kukatia tiketi wa N-Card, waziri huyo alisema tayari timu zimeshafanya uchambuzi wa changamoto hiyo na serikali inakwenda kuyafanyia kazi.

Bashungwa aliagiza pia, TEMESA kuhakikisha wananchi wote wanaopata huduma za vivuko katika eneo la Magogoni-Kigamboni wawe wanalipa nauli kama mchango kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa huduma hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameeleza kuwa taasisi nyingi zilizoko mkoani humo zinafanya kazi kubwa na ameitaka pia TEMESA kuongeza ushirikiano na mkoa kwa kuwa wanajihusisha moja kwa moja na wananchi.

Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kilahala, alisema kwa sasa Kituo cha Magogoni-Kigamboni kina vivuko viwili MV Kazi na MV Kigamboni vinavyotoa huduma za uvushaji kwa saa 24 na kufanfua kuwa, kivuko cha MV Magogoni ambacho kimepelekwa kwenye matengenezo makubwa, utekelezaji umefikia asilimia 55.2.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Huduma za Kisheria (LSF), Lulu Ng'wanakilala (kulia) na Mtendaji Mkuu wa Benki ya Stanbic, Manzi Rwegasira, wakitiliana saini makubaliano ya ushirikiano jijini Dar es Salaam jana, unaolenga kuwawezesha wanawake na wasichana katika afya, elimu, ujuzi wa masuala ya fedha na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, masuala ya mazingira na hali ya hewa, ukiangazia mtazamo wa kina wa maendeleo endelevu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Ugonjwa wa figo unaweza kudhibitiwa'

**Na Christina Mwakangale**

TATIZO la ugonjwa wa figo linaendelea kuwakumba watu wengi nchini likiwa ni kati ya magonjwa yasiyoambukiza yenye kutumia gharama kubwa za matibabu.

Ugonjwa sugu wa figo (CKD) ni hali inayomkumba mtu baada ya figo zake kutofanya kazi ipasavyo na kuhitaji kusafishwa kila baada ya siku tatu kwa wiki.

Tovuti ya National Health Service (NHS) ya nchini Uingereza inayotoa elimu kuhusu afya, inasema ugonjwa huo unaweza kumwathiri mtu yeyote licha ya kubainika kuathiri zaidi watu weusi na wenye asili ya Asia Kusini.

Wanaougua ugonjwa huo wanaweza kuishi kwa muda mrefu na hali hiyo licha ya figo kutofanyakazi.

**DALILI**

Tovuti hiyo inabainisha kwamba kwa ujumla hakuna dalili za moja kwa moja katika hatua za awali, bali tatizo linaweza kugundulika kupitia damu au mkojo.

Mtu anaweza kwenda hospitali kufanyiwa vipimo vya damu na mkojo akihisi kuugua ugonjwa mwingine, anaweza kutoka pia na majibu kwamba kuna uwezekano wa tatizo la figo.

Katika hatua zinazofuata mtu anaweza kuhisi ana uchovu, kuvimba vifundo, miguu au mikono, kuhisi yu mgonjwa, sukari kuwamo katika mkojo na kupungukiwa damu.

**SABABU ZA UGONJWA**

Sababu za ugonjwa wa figo huchangiwa na athari zinazofikia figo na kusababisha matatizo moja wapo ni shinikizo la damu ambalo linaweza kuleta mgandamizo kwenye damu na figo kutofanya kazi vizuri.

Kisukari pia huchangia figo kutatizika. Kiwango cha sukari (glucose) kikiwa juu kinaweza kuathiri chujio za kwenye figo na kuathiri utendaji kazi.

Pia, ugonjwa wa figo husababaishwa na maambukizi kwenye kiungo hicho na baadhi hurithi ugonjwa, matumizi ya muda mrefu, kama vile lithiamu na dawa zisizo za steroidal za kuzuia vichochezi (NSAIDs).

NHS inashauri kwamba kuepuka tatizo la figo ni kubadili mtindo wa maisha kwa kudhibiti sababu za ugonjwa huo.

**Tovuti ya National Health Service (NHS) ya nchini Uingereza inayotoa elimu kuhusu afya, inasema ugonjwa huo mara nyingi unahusishwa na umri mkubwa.**

Uchunguzi wa mara kwa mara unashauriwa ili tatizo liweze kubainika mapema.

**TIBA**

Matibabu ya ugonjwa sugu wa figo hakuna yaliyo halisi ingawa kupunguza dalili kutofikia hali mbaya inasaidia.

Pia, upandikizaji wa figo unaweza kuwa muhimu na inashauriwa kuwa na ukaguzi wa mara kwa mara.

Dalili za ugonjwa huo zinaweza kuanza taratibu watu wengi walio nao wanaweza kudhibiti hali zao kwa kutumia dawa na uchunguzi wa mara kwa mara.

Kati ya watu 100, wawili wanaweza kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Wanaougua ugonjwa wa moyo na mishipa ni kundi linaloathiriwa zaidi, ingawa tiba ya dawa na kubadili mtindo wa maisha kunaweza kuepuka ugonjwa huo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Mchuuzi wa dagaa akimhudumia mteja wake katika mnada wa soko la samaki la Kimataifa la Magogoni maarufu Feri, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kwa mujibu wa wavuvi, kitoweo hicho, kimekuwa adimu sokoni hapo kutokana na hali ya hewa mbaya baharini inayosababishwa na msimu wa mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mwigulu aomba WB kuongeza fedha IDA21

**Josephine Majura na Saidina Msangi,**
NAIROBI

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema kuna umuhimu wa kuongeza fedha kwenye dirisha la Mzunguko wa 21 wa Mfuko Maalumu wa Maendeleo wa Benki ya Dunia (IDA21) ili kufikia malengo ya utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya Afrika.

Akizungumza katika mkutano wa IDA21 unaoendelea jijini Nairobi uliowaleta pamoja wakuu wa nchi za Afrika, mawaziri na viongozi wengine, alisema mzunguko huo unatarajiwa kuanza Julai 2025 hadi Juni 2028.

"Hili dirisha limekuwa likitoa mikopo kwa masharti nafuu, riba kwa kiwango cha chini na muda wake wa kurudisha umekua mrefu ambapo Tanzania kwa kiwango kikubwa inatumia dirisha hilo kupata fedha zinazotumika kuendeleza sekta za huduma za jamii kama vile elimu, maji pamoja na umeme kwa bei nafuu," alisema.

Aidha, dirisha hilo ambalo riba ya mikopo yake haizidi asilimia mbili, limekuwa likitoa mikopo kwa nchi za Afrika yenye masharti nafuu ili kuzipunguzia kupata mikopo kutoka benki za kibiashara ambayo huwa na gharama kubwa.

Dk. Nchemba alisema kuwa mkutano huo utasisitiza umuhimu wa kupatikana kwa fedha za IDA kwa ajili ya kuzisaidia nchi kutoka katika athari za majanga na kuwezesha kurejea katika hali ya kawaida kwa ajili ya maendeleo endelevu Afrika.

Jana Rais Samia Suluhu Hassan alihutubia mkutano huo, pia umehudhuriwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango-Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu El Maamry Mwamba, Kamishna wa Fedha za Nje Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Yussuf Ibrahim Yussuf na viongozi wengine.

# MNMA yapata ubalozi mradi Usalama Kwanza dhidi VVU

**Na Romana Mallya**

CHUO cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kimechaguliwa kuwa balozi wa vyuo vikuu Tanzania katika Mradi wa Usalama Kwanza uliolenga kufikisha elimu ya kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI kwa wanafunzi wasichana wa vyuoni.

Uchaguzi huo umefanywa na Jumuiya ya Kimataifa ya Wanawake Wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) Ukanda wa Afrika Mashariki (ICWEA), kupitia Shirika linalojishughulisha na masuala ya Utu na Ustawi wa Wanawake Wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (DWWT).

Katika mafunzo ya kuwajengea uwezo baadhi ya wanafunzi wa MNMA na vinara sita (Champion) waliochaguliwa mwishoni mwa wiki, Mratibu wa mradi huo, Bahati Haule, kutoka DWWT, alisema mradi umechagua wasichana vinara sita kutoka MNMA.

Haule alisema wasichana hao watahamasisha wanafunzi wengine katika mradi huo.

Alisema katika mafunzo hayo wanafunzi hao wamefundishwa uelewa wa masuala ya VVU na UKIMWI sambamba na umuhimu wa kujua hali zao kiafya.

Haule alisema pia wanafunzi hao wamepatiwa elimu ya kuwahamasisha wenzao umuhimu wa kupima afya zao ili kujua hali zao kiafya.

Mwakilishi kutoka Jumuiya ya Kimataifa ya Wanawake wanaoishi na Maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi Ukanda wa Afrika Mashariki (ICWEA), Dk. Tatu Nyange, alisema MNMA kimebahatika kupata fursa ya pekee katika kuviwasilisha vyuo vikuu vyote vilivyoko nchini.

Alisema ICWEA ambayo ina matawi katika nchi tano za Ukanda wa Afrika Mashariki ikiwamo Tanzania, imeona ni muhimu MNMA ikashiriki katika mradi huo na kuviwakilisha vyuo vingine vilivyoko nchini.

Alisema mradi huo utavihusisha vyuo viwili kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki ambavyo ni MNMA kutoka Tanzania na Makerere cha Uganda.

Dk. Nyange alitaja nchi nyingine wanachama wa ICWEA kuwa ni pamoja na Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

Alisema ICWEA inaamini kuwa, tofauti za kijinsia na ukosefu wa afya ya uzazi na haki za binadamu kwa wanawake, ni msingi wa janga la UKIMWI na VVU.

"Imetambuliwa kwamba, UKIMWI una sura ya mwanamke kwa bahati mbaya wanawake bado hawapo katika michakato ya uamuzi inayofanywa kuhusu sera, programu na sheria za UKIMWI ambazo zitakuwa na athari kwa maisha na ustawi wa wanawake," alisema.

Alisema uanachama wa ICWEA unategemea watu binafsi na usajili wa wanachama ni bure kwa wanawake wanaoishi na VVU.

Mkurugenzi wa Huduma za Wanafunzi Ukende Mkumbo akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Chuo, Prof. Shadrack Mwakalila, aliishukuru DWWT na ICWEA kwa kukichagua chuo hicho katika mradi huo ambao umelenga vijana hususan wa kike, kujua hali zao na kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Alisema pamoja na mradi huo kulenga wasichana vinara sita, kufikisha elimu hiyo kwa wenzao, lengo likiwa kufikia wasichana wengine 600, na hiyo itawezekana kwa ushirikiano wa wanafunzi, uongozi wa chuo na zahanati iliyoko chuoni hapo.

Alisema uongozi wa chuo uko tayari kushirikiana kwa hali na mali ili elimu hiyo kwa wasichana ilete tija na kupunguza idadi ya wanafunzi ambao hawajua hali zao za kiafya.

Alisema sasa wataipata kupitia elimu ya ushawishi watakayopatiwa na wenzao ambao tayari ni vinara wa mradi wa usalama kwanza.

Ismail Mohamed, ambaye ni Mratibu wa masuala ya Virusi vya Ukimwi na UKIMWI (CHAC), Wilaya ya Kigambon, alisema serikali iko pamoja na mradi huo ambao umelenga kulinda afya ya vijana hususan wasichama na kwamba, ipo tayari kutoa ushirikiano utakapoitajika.

# TAKUKURU yawabana wakopaji, warejesha mamilioni ya fedha

**Na Oscar Assenga,** TANGA

ZAIDI ya Sh. milioni 439.27 za mikopo inayotokana na ruzuku ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, imerejeshwa serikalini baada ya wanufaika waliogoma kurejesha kubanwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Fedha hizo ni kati ya Sh. bilioni 2,152.229 zilizokuwa hazijarejeshwa kwa wakati kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa TAKUKURU mkoani hapa, Victot Swella, miongoni mwa mambo waliyobaini katika ufuatiliaji wa fedha hizo ni kukiukwa kwa masharti ya kurejeshwa mikopo hiyo.

Ufuatiliaji huo ni utendaji kazi wa TAKUKURU wa kipindi cha kati ya Januari hadi Machi mwaka huu.

Alisema baada ya kulibaini hilo, taasisi hiyo iliwakutanisha wadau na kuweka mapendekezo ya kurejesha fedha hizo na hadi kufikia Februari mwaka huu, Sh. milioni 439,279,300.00 zilirejeshwa katika halmashauri hiyo.

Hadi sasa Sh. 1,712,950,600 hazijarejeshwa na kwamba jitihada za ufuatiliaji zinaendelea.

Vilevile katika kipindi hicho, walifuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo 46 yenye thamani ya Sh. 8,041,998,680.00 katika sekta za elimu, barabara, maji na afya.

Katika ufuatiliaji huo walibaini miradi 32 yenye thamani ya Sh. 4,866,068,966.00 ina mapungufu na kushauri kurekebisha kupitia vikao na wadau husika.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kulia), akizungumza jambo alipotembelea banda la Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kwenye Maonyesho ya Wiki ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) katika uwanja wa General Tyre, Njiro, jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma na (katikati) ni Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkataba kampuni ununuzi mwani hatarini kuvunjwa

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SERIKALI mkoani hapa imesema itavunja mkataba na kampuni zinazokiuka makubaliano ya kuwakopesha wakulima wa mwani pembejeo za kilimo.

Msimamo huo ulitangazwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Burian, wakati akizungumza na wafanyabiashara na kampuni zinazonunua zao hilo.

Ni baada ya kuwatembelea wakulima wa zao hilo katika wilaya za Muheza, Tanga, Mkinga na Pangani walioingia makubaliano hayo na kampuni hizo ya kukopeshwa pembejeo hizo.

Balozi Buriani, alisema haiwezekani wanunuzi wa zao hilo wakaingia mkataba na wakulima na kushindwa kutoa pembejeo hizo na kusababisha wahangaike.

"Ninyi wanunuzi kama hii kazi imewashinda tutavunja mikataba na turudi kwa wakulima wetu na tuwaambie Benki ya Kilimo watoe mikopo yenye riba chini ya asilimia nne mpaka tatu," alisema na kuongeza kuwa: "Tunajua kabisa wakikopeshwa wanaweza kununua kamba, taitai na troliki na kufanya kilimo chenye tija na faida."

Awali, Ofisa Mfawidhi wa Idara ya Ukuzaji wa Viumbe Maji, Mkoa wa Tanga, Omari Mohamed, alisema serikali imekuwa ikisaidia na kusimamia na kuna mikopo ambayo haina riba. Mohamed, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi inashirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kuwakopesha wakulima hao pembejeo na boti za uvuvi.

Alisema awamu ya kwanza ilikwisha kufanyika na wapo kwenye awamu ya pili. "Awamu ya pili tutatoa pembejeo kwa wakulima wa mwani nchi nzima."

Hata hivyo, alisema kwa sasa serikali inaangalia sehemu zenye mapungufu ili iweze kusaidia.

## GGML yapongezwa kudhibiti vifo kazini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameipongeza Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kudhibiti matukio ya vifo na majeruhi katika shughuli za uchimbaji mgodini na kuwataka waajiri wengine kulinda usalama wa waajiriwa wao.

Dk. Biteko alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kutembelea banda la GGML katika maonesho ya afya na usalama mahali pa kazi yanayoendelea Viwanja vya General Tyre jijini Arusha.

Biteko ambaye pia alikuwa mgeni rasmi katika kilele cha maonesho hayo, alieleza kufurahishwa na elimu ya afya na usalama mahali pa kazi inayotolewa na washiriki.

"Niwapongeze wale mliofanya maonesho hapa, mmetoa elimu kubwa kwangu na kwale ambao tumepita, lakini tumejifunza bado zipo kazi za kufanya," alisema.

Alisema waajiriwa wanatakiwa kuzingatia usalama na afya mahali pa kazi kwani kifo cha mtu mmoja kwa takwimu ni sawa na asilimia 100 kwa wategemezi wake ambao ni mke, watoto, ndugu na majirani.

"Kifo cha mtu mmoja ni kikubwa, kinatakiwa kisitokee. Wito kwa waajiri wote wakati wote ninataka mhakikishe mnarekodi sifuri katika matukio haya ya vifo mahali pa kazi.

"Kwa waajiriwa wito wangu kwenu ni kwamba mtu wa kwanza kulinda usalama ni mwajiriwa mwenyewe, ukiona mtambo unaopaswa kuundesha na una kasoro huku ukiwa umelazimishwa na mwajiri kuuendesha, uwe wa kwanza kusema mtambo huu haupo salama na usihesabike kuwa mtu uliyegoma kwa sababu pia una wajibu kulinda usalama wako," alisema.

Alitoa wito kwa kila mtu kuthamini maisha yake pindi anapokuja kazini anarejea salama bila kuwa na madhara yoyote.


Awali akimkaribisha Dk. Biteko katika banda la GGML, Meneja Usalama wa kampuni hiyo, Isack Senya alisema kuwa kwa kipindi cha zaidi ya miaka 15 halijatokea tukio la vifo kwa mfanyakazi akiwa kazini.

Senya alimwelezea Dk. Biteko namna GGML inavyotumia mfumo wa rada kuangalia mienendo ya miamba au kuta katika maeneo ya uchimbaji.

Pia alimweleza kuwapo chumba maalum cha uokozi chini ya ardhi katika migodi ili kufanya uokozi kunapotokea dharura.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), Hadija Mwenda alisisitiza wataendelea kusimamia majukumu yao ipasavyo kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa.

"Tutaendelea kuwezesha maeneo ya kazi yawe salama. Suala la usalama na afya ni suala la kujenga tabia na ujengaji tabia ni jambo linatokana na kuelimishwa," alisema.





# Wazazi wachangia wanafunzi kukithiri utoro

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Ng'homango wilayani hapa wanadaiwa kukithiri kwa utoro kwa kuzuiwa na wazazi wao kwenda shule msimu wa kilimo.

Madai hayo yalitolewa juzi na Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, Peter Yuga wakati akizungumza na Nipashe shuleni hapo kuhusiana na mahudhurio ya wanafunzi.

Yuga, alisema katika msimu huo wa kilimo, baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwazuia kwenda watoto wao kwenda shule na kuwapeleka mashambani kulima.

Mtendaji wa Kijiji hicho cha Ng'homango, Madilya Nyema, alisema kutokana na kukithiri kwa utoro wa wanafunzi msimu huu wa kilimo, waliitisha mkutano wa hadhara na kuwaonya wazazi kuwa mwanafunzi atakayekutwa shambani wakati wa masomo atatozwa faini ya Sh.10,000.

Nyema, alisema licha ya kuweka faini hiyo wazazi waliendelea kukaidi amri hiyo na kuendelea kuwazuia watoto wao kwenda shule.

Alisema kiasi cha fedha walizokuwa wakikusanya kwa kutoza faini hilo, zilielekezwa kwenye ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shuleni hapo.

"Baada ya kuona wazazi wamekuwa vichwa ngumu na kuona faini hiyo ni kidogo, tukaamua kuongeza faini kuwa ni kupeleka shuleni hapo mifuko miwili ya saruji kwa kila kichwa cha mtoto, sasa hivi utoro umepungua siyo kama zamani," alisema.

Baadhi ya wanafunzi shuleni hapo walithibitisha baadhi ya wazazi kuwazuia kwenda shule msimu wa kilimo na kusababisha kukithiri kwa utoro.

Mmoja wa wazazi, Razalo Masanyiwa, alisema baadhi yao wanawazuia watoto kwenda shule ili wakalime mashambani wakati wa kilimo na mavuno kutokana na uchache wa watu kwenye familia.



Mwenyekiti wa Bodi ya JTI Leaf Services, Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda (wa tatu kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. milioni 150 kwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Maendeleo Urambo (UDEI) na Mbunge wa Urambo, Margret Sitta kwa ajili ya ujenzi wa bweni jipya, wakati wa hafla ya kukabidhi rasmi bweni la Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Margret Sitta, wilayani Urambo, mkoani Tabora mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Marekani kupambana malaria Tabora

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MFUKO wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI) umeahidi kuongeza msaada wa utoaji huduma kwa Mkoa wa Tabora ili kupunguza kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo.

Hayo yalibainishwa na Mwakilishi wa Shirika la Misaada la Kimataifa Marekani (USAID) nchini, Lulu Msangi wakati akiwasilisha taarifa ya shirika hilo kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani yaliyofanyika Kitaifa mkoani hapa .

Lulu alisema kuwa mradi huo unaojulikana kwa jina la PMI Shinda Malaria utaanza kutekelezwa na Taasisi ya Ifakara Health Institute (IHI) kwa ufadhili ya USAID baada kuzinduliwa katika maadhimisho hayo.

Alisisitiza kuwa msaada huo utajumuisha afua ya uchunguzi wa malaria na matibabu, afua ya mabadiliko ya tabia za kijamii, kuzuia malaria wakati wa ujauzito, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za kupambana na ugonjwa huo.

Lulu alibainisha kuwa shirika hilo halifurahishwi na kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo mkoani hapa kutokana na utafiti kubaini umewapata asilimia 23 ya watoto walio chini ya miaka mitano.

'Hiki ni kiwango kikubwa sana cha malaria ukilinganisha na viwango vya mikoa ya Singida, Manyara, na Dodoma ambayo ina asilimia moja tu ya watoto chini ya umri huo waliopatikana na ugonjwa huo," alisema.

Mkurugenzi wa Miradi Wizara ya Afya, Cathylene Joachim, alisema serikali imeendelea kuweka mkazo na hamasa ya kudhibiti maambukizi hayo katika mkoa huo na mingine yenye kiwango kikubwa nchini.

Alitaja makundi mengine ambayo yako katika hatari kubwa ya kupata malaria kuwa ni wajawazito, wafanyakazi migodini, wavuvi na wakulima, hivyo wataendelea kuongeza hamasa zaidi kwenye matumizi ya vyandarua.

Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanaharakati wa Kupambana na Malaria (TAPAMA), Riziki Lulinda, aliishauri serikali kuja na mkakati madhubuti wa kudhibiti ugonjwa huo mkoani hapa.

Akihitimisha maadhimisho hayo, Naibu Waziri wa Afya. Dk. Godwin Mollel aliwataka wakazi wa Tabora na mikoa mingine nchini kutumia vyandarua na wanapohisi kuwa na malaria waende hospitalini.

Kwa mujibu wa Dk. Mollel, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameipatia wizara hiyo takriban Sh. tril. 6.7 kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo ili kuhakikisha kiwango kinashuka hadi asilimia 3.5.

Alisema kiwango cha malaria kinaendelea kupungua kila mwaka kwani mwaka 1990 maambukizi yalikuwa asilimia 50 lakini sasa wana asilimia 8.1 kitaifa licha ya mkoa huo kuwa na asilimia kubwa.

## Halmashauri zashindwa kukusanya kodi ya uzio

**Na Rose Jacob,** MWANZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza imesema halmashauri mkoani hapa zimeshindwa kukusanya kodi ya zuio kwa wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, James Ruge, alisema kuwa tatizo hilo linachangia kushuka kwa makusanyo ya mapato.

"TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imefanya kazi ya uchambuzi wa mfumo wa kodi ya zuio na kufanikiwa kukusanya zaidi ya Shilingi milioni 68.164 katika halmashauri ya Ilemela kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)," alisema Ruge.

Alisema taasisi hiyo pia imebaini mapungufu mbalimbali ikiwemo uelewa mdogo kwa wafanyabiasharawa kodi hiyo ya zuio na baadhi ya watoa huduma mitaani hususani mafundi ujenzi kutokuwa na namba ya mlipa kodi (TIN).

# Ujio madaktari bingwa upasuaji, figo kuleta neema kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

MADAKTARI bingwa kutoka Uturuki wamewasili nchini kwa ajili ya kutoa matibabu ya upasuaji kwa wagonjwa mbalimbali, ikiwamo upandikizaji wa figo, utengenezaji wa mishipa ya njia ya damu, upasuaji wa uvimbe, matiti, nyongo, magonjwa ya njia ya haja kubwa na mfumo wa chakula ambao wataweka kambi katika Hospitali ya Shifaa Pan Africa iliyoko wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa East Africa Afya Turkish Healt Services, Fatih ilhan, alisema juzi kuwa huduma hizo za upimaji kwa wagonjwa zitatolewa bure bila malipo kwa wananchi wote.

"Kambi hiyo inawalenga watu wazima na watoto wenye viashiria vya magonjwa ya figo na moyo, ikiwamo, kutoongezeka uzito, kupumua kwa shida, kuchoka, kikohozi cha mara kwa mara, kutokwa jasho jingi pamoja na kushindwa kuhimili mazoezi." Alisema.

"Natoa wito kwa ambao waoonesha viashiria kama hivyo wafike hospitalini hapa, tunawafanyia uchunguzi bila malipo, wenye kuhitaji tiba watazipata," alisema. Aidha, Kampuni ya East Africa Afya Turkish Healt Services inayoratibu kambi hiyo ya madaktari kwa kushirikiana na Vertex Group Experts, inawaarifu wananchi wote wenye matatizo mbalimbali yanayopaswa kufanyiwa upasuaji na wenye matatizo ya figo kufanya utaratibu mapema wa kupata nafasi ya matibabu kuanzia Mei 1, mwaka huu ili kuonana na madaktari bingwa ambao ni Prof. Dk. Soykan Barlas (bingwa wa upasuaji) na Prof. Dk. Suheyla Apaydin (daktari bingwa wa magonjwa ya figo). Pia alisema kambi itakuwa ni ya siku moja tu ila Kampuni ya East Africa Afya Turkish Healt Services itaendelea kufungua milango kwenye ofisi zake kwa wiki nzima kutoa ushauri kwa wagonjwa mbalimbali wanaotafuta huduma ya kitabibu katika hospitali zilizoko Uturuki, alisema ofisi zitakuwa wazi kuanzia saa 02:00 asubuhi hadi saa 09:30 mchana, hivyo aliwahimiza wananchi kuchangamkia fursa hiyo.

Mkazi wa Kinondoni, Najma Ismail, aliyewahi kufika katika hospitali hiyo mwenye maradhi ya figo amefurahishwa na huduma alizozipata.

"Nimepokelewa vizuri, nimepata huduma vizuri naupongeza uongozi wa Shifaa kwa kuandaa kambi hii ya matibabu ya figo ya bure kwa sababu itatupa fursa ya kukutana na madaktari bingwa," alisema.

Naye Peter Mwalongo Mkazi wa Nkuhungu mkoani Dodoma, alisema amepata taarifa ya kambi hiyo kupitia mitandao ya kijamii na amejipanga kuja Dar es Salaam kupata huduma hiyo ya bure.

Nimeishi na taatizo la figo kwa muda mrefu fursa hii itanipa mimi nafasi ya kukutana na wataalamu wa uhakika nitaambatana na mke wangu alituambia ili naye aweze kutumia fursa hiyo kufanyiwa uchunguzi bure kwa kuwa unafanyika bure.

"Kambi hii ni fursa kwa watu wengi hasa wasiyojiweza kwa kuwa inatoa nafasi kwao kupata huduma za kibingwa bure, hivyo naupongeza uongozi wa Hospitali ya Shifaa na Kampuni ya East Africa Afya Turkish Healt Services kwa kuleta kambi hii." Alisema.

## Tuhuma ubadhirifu mawaziri wafungiwa kuondoka DRC

**KINSHASA,** DRC

MAWAZIRI watatu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), akiwamo wa fedha, na waziri wa zamani wamepigwa marufuku kuondoka nchini humo kutokana na kuhusishwa na tuhuma za ubadhirifu wa fedha za umma, jambo ambalo tayari linachunguzwa na mahakama.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Firmin Mvonde, anawataka maofisa wa Kurugenzi Kuu ya Uhamiaji (DGM) kuwapiga marufuku kuondoka Kinshasa na kwenye ardhi ya Kongo.

Mawaziri hao wa Fedha na Maendeleo ya Vijijini ni Nicolas Kazadi (pichani) na François Rubota mtawalia, pamoja na Waziri wa zamani wa Maendeleo ya Vijijini, Guy Mikulu.



Chanzo kilichoko karibu na Nicolas Kazadi, kilibainisha kuwa kiongozi huyo alipigwa marufuku Jumamosi kuondoka Kinshasa kuelekea Ufaransa, ambako Rais wa DRC, Félix Tshisekedi, yuko katika ziara rasmi ya siku mbili Jumatatu na Jumanne.

Katika barua nyingine iliyotumwa kwenye mitandao ya kijamii ambayo uhalisi wake haukuweza kuthibitishwa mara moja, Kazadi mwenyewe alimtaka Mwanasheria Mkuu wa serikali Mvonde kuchunguza tuhuma za kutoa bili ya fedha kupita kiasi katika mkataba wa uchimbaji visima na vituo vya kusafisha maji nchini humo.

Pia alipendekeza uchunguzi ule ule katika kesi nyingine ya madai ya bili ya pesa kupita kiasi, kuhusu uwekaji wa taa za barabarani mjini Kinshasa.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, Kazadi hakuweza kupatikana ili kutoa maoni yake. Lakini alihojiwa kuhusu faili hizo mbili wakati wa mkutano uliofanyika Aprili 24 pamoja na msemaji wa serikali, uliojikita katika majadiliano ya DRC na taasisi za fedha za kimataifa.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa alikanusha ukiukwaji wowote, akidai kinyume chake aliomba pande zinazohusika katika mikataba hiyo kupunguza gharama zao. "Ikiwa kuna watu waliotoza pesa za kupita kiasi, hakika sio mimi," alisema juu ya uchimbaji visima, na kusema ana huzuni kwa uhusishwa na uvumi huo. **RFI**

# Mashtaka yaliyokuwa yakimkabili Rais Akufo-Addo Ghana yafutwa

**ACCRA,** Ghana

MAHAKAMA kuu nchini Ghana imefuta mashtaka yaliyokuwa yakimkabili Rais wa nchi hiyo, Nana Akufo-Addo ya kushindwa kuchukua hatua za haraka kuhusiana na mswaada unaopinga ushoga iliyopitishwa na Bunge Februari, mwaka huu.

**Mbunge mmoja wa upinzani, Rockson-Nelson Dafeamekpor, aliwasilisha ucheleweshaji wa sheria hiyo mahakama kuu, ambayo imetoa hukumu dhidi ya malalamiko yake juzi.**

Ilibainishwa kuwa awali wabunge kwa idadi kubwa walipitisha sheria ambayo itaongeza ufuatiliaji wa haki za mashoga katika taifa hilo la Afrika Magharibi, na kwamba wamekuwa wakimshinikiza Rais Akufo-Addo atangaze sheria hiyo mpya.

Ilieleza kuwa ofisi ya rais ilisema hautaupeleka mswaada huo kwa rais kuidhinishwa mpaka mashtaka hayo mawili dhidi yake yasuluhishwe, hoja ambayo inatajwa kuzua ukosoaji bungeni.

Mbunge mmoja wa upinzani, Rockson-Nelson Dafeamekpor, aliwasilisha ucheleweshaji wa sheria hiyo mahakama kuu, ambayo imetoa hukumu dhidi ya malalamiko yake juzi.

Jaji Lordina Mireku, alisema mahakama imefanya uamuzi haitakuwa sahihi kumlazimisha kiongozi mkuu wa taifa hilo kushughulikia sheria ambayo inapambana na changamoto mbili za kisheria katika mahakama kuu. Huku mwanasheria wa Dafeamekpor akisema atakata rufani dhidi ya hukumu hiyo.

Aidha, ilibainishwa kuwa watu wenye uhusiano wa mapenzi ya jinsia moja nchini Ghana tayari wanakabiliwa na adhabu ya kifungo cha hadi miaka mitatu jela.

Iwapo sheria hiyo itaanza kufanya kazi, itaongeza muda wa kifungo jela na ufutiaji wa haki za mashoga na wanatuhumiwa kuukuza utambulisho wa mashoga, wasagaji na makundi mengine ya watu wachache au utambulisho wa kijinsia. **VOA**



Hali ya mafuriko ilivyo nchini Kenya. **PICHA: MTANDAO**

# 50 wauawa baada ya bwawa kupasuka

**NAIROBI,** Kenya

TAKRIBANI watu 50 wamefariki dunia nchini Kenya baada ya bwawa lililoko kaskazini mwa mji mkuu Nairobi kupasuka, wakati nchi hiyo ikiendelea kukumbwa na mvua kubwa zinazoleta mafuriko na kusababisha uharibifu wa miundombinu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Msalaba Mwekundu nchini humo, bwawa hilo lilipasuka juzi huko Mai Mahiu, Kaunti ya Nakuru, na kwamba hiyo ilitokana na mvua kubwa iliyonyesha usiku kucha na kusababisha lango la bwawa hilo kuharibika kutokana na kuzidiwa na maji.

Ilielezwa kuwa hali hiyo ilisababisha madhara zaidi katika kijiji cha Ngueiya ambako kulitokea maporomoko makubwa ya matope, miti kung'olewa, huku mawe yakiporomoka kutoka mlimani hadi kwenye makazi ya watu.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo Joseph, alisema "Ilikuwa karibu saa 9 usiku ambako mafuriko yalipiga nyumba yangu, nilikuwa kitandani kwangu na nikasikia sauti ya nje. Nilitaka kutoka lakini mlango wangu ulizuiwa na maji. Maji yalijaa katika nyumba yangu, ghafla ikasombwa. kila kitu kikazamishwa majini hata kuta, akuna kilichobaki".

Anna anayetoka katika kijiji cha Jerusalemu, alisema familia yake ndiyo pekee iliyookoka wakati maji ya mafuriko yalipowachukua watoto wake, na kwamba alifikiri kuwa hatawaona tena.

"Walisombwa na maji. Sote tulitenganishwa. Nilisikia watoto wangu wakipiga kelele kwa mbali. Baada ya kama dakika ishirini nilianza kuogelea. Nilimkuta binti yangu mmoja amelala juu ya mti, nikamuokoa. Niliogelea tena kumchukua binti yangu mwingine," alisema.

Ilielezwa kwa wakati huo, hakua na matumaini ya kuwapata waathirika. Wakati waokoaji na majirani wakiendelea kutafuta miili ya watu waliotoweka. Huku David Aderasu, kutoka shirika lisilo la kiserikali la 'Saint John Ambulance' akisema alipata watu kadhaa waliofariki.

"Nilipata miili hapa, kuelekea Mai Mahiu chini, kwa sababu ilibebwa na maji. Baadhi walikuwa wakielea, wengine walikuwa wamekwama kwenye matope. Kuna timu nyingine, chini kidogo, inaendelea kuchimba kuopoa miili ambayo bado imekwama," alisema.

Kwa mujibu wa Shirika la Msalaba Mwekundu la Kenya, watu 49 bado hawajapatikana.

Aidha, ilielezwa kuwa si mara ya kwanza kwa kaunti ya Nakuru kushuhudia janga kama hilo, na kwamba mwaka 2018, kuporomoka kwa bwawa la Solait kulisababisha karibu watu 50 kuathirika baada ya mvua kubwa iliyosababisha mafuriko na uharibifu.

Hata hivyo, Waziri wa Mambo ya Ndani nchini Kenya, alitangaza kuwa mabwawa yote yatafanyiwa ukaguzi ndani ya saa 24. kwasababu mvua zinaendelea na vimbunga vikali vinatarajiwa.

Vile vile kutokana na hali hiyo ufunguzi wa mwaka wa shule uliokuwa umepangwa kufanyika Aprili 29 umeahirishwa kwa wiki moja.

Katika hatua nyingine, ilibainishwa kuwa Rais William Ruto, aliitisha kikao maalum cha baraza la mawaziri kujadili hatua za kukabiliana na mafuriko ambayo yamesababisha vifo vya zaidi ya watu 170 kote Kenya na wengine 185,000 kuhama makazi yao. **RIF**

HABARI MICHEZO

# ILAMFYA SASA ATAKA NGUVU ZAIDI MTIBWA, KINACHOIUA CHAANIKWA

Faustine Feliciane na Adam Fungamwango

WAKATI mshambuliaji wa Mtibwa Sugar, Charles Ilamfya, akikiri timu hiyo kuwa kwenye wakati mgumu na kuwataka wachezaji wenzake kuongeza nguvu zaidi na kuhakikisha wanaipambania ili isishuke daraja, mmoja wa kiongozi wa timu hiyo ameanika kinachoimaliza timu hiyo msimu huu.

**Mtibwa Sugar inaburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 17 pekee baada ya kucheza michezo 26.**

Mchezo wao uliopita, Mtibwa imekubali kipigo cha mabao 2-1 mbele ya JKT Tanzania juzi katika Uwanja wa Meja Isamuhyo uliopo Mbweni, Dar es Salaam.

Ilamfya alisema wanahitaji kuongeza nguvu zaidi kwenye michezo iliyobakia ili kuinusuru timu hiyo na janga la kushuka daraja kutokana na nafasi hiyo waliopo kwa sasa.

"Hatuna matokeo mazuri, tunahitaji nguvu ya ziada kuhakikisha tunainusuru timu, lazima tuongeze nguvu kama wachezaji kwenye michezo iliyobakia," alisema nyota huyo wa zamani wa Simba.

Alisema matokeo wanayoyapata yanawaumiza kama wachezaji kwa kuwa lengo lao ni kuona timu inafanya vizuri na inabaki Ligi Kuu msimu ujao.

Aidha, alisema anaamini mechi zinazofuata watapambana zaidi na kuhakikisha wanapata alama tatu muhimu.

Katika mchezo huo uliopita, bao pekee la Mtibwa lilifungwa na Ilamfya ingawa halikutosha kuwaondolea kipigo kutoka kwa wanajeshi hao ambao mabao yao yalifungwa na Edson Katanga dakika ya saba na Sixtus Sabilo dakika ya 90.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Klabu ya Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, amekiri wana hali mbaya, akisema kinachotakiwa sasa ni sala na maombi kwa wote wanaoitakia mema timu hiyo ili ibaki Ligi Kuu, pia akibainisha kuwa matatizo ya timu hiyo yanatokana na kujiweka pembeni kwa aliyekuwa mratibu wake, Jamal Bayser.

"Matokeo si mazuri, kwetu ni mabaya mno, tumefanya uzembe kwenye mchezo wa leo, tumeruhusu bao jepesi dakika ya 90. Sasa tuangalie benchi la ufundi litafanya nini katika michezo iliyobaki, ila lazima tuelezane ukweli, tunaweza kupotea katika Ligi Kuu Tanzania Bara, tunachohitaji zaidi ni sala na maombi kutoka kwa wadau na mashabiki wa soka ambao wana mapenzi mema na Mtibwa pamoja na soka la Tanzania," alisema Kifaru.

Alibainisha sababu za Mtibwa kutofanya vema katika misimu ya hivi karibuni ni kutokana na kujiweka pembeni kwa aliyekuwa mratibu wake.

"Niseme tu tangu kukaa pembeni kwa mratibu Bayser, ambaye alikuwa na klabu hii tangu 1998 na kufanya makubwa, baada ya kutoka tumekuwa na watendaji ambao bado tunapata nao shida, hatujawa na watendaji wazuri kama yeye, kukaa kwake pembeni ni pengo kubwa sana, hatuna mtu sahihi, ndicho kinachosababisha tuwe na hali hii," alilalamika Ofisa Habari huyo.

Ikiwa imebakisha mechi saba, Mtibwa bado inaburuza mkia ikiwa na pointi 17, huku ikibakisha mechi zake za nyumbani dhidi ya Azam FC, Yanga, Namungo na Tabora United, na za ugenini ni dhidi ya Simba, Mashujaa FC na Ihefu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi cheti cha udhamini, Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano wa KCB Bank Tanzania, Christina Manyenye, wakati wa mbio za usonji (Run4Autism Marathon), zilizofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## KVZ FC kutumia mbinu Simba kuiua Kipanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ FC imesema inakikosi kipana kitakachowapa matokeo mazuri katika mchezo wao mzunguko wa 21 Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Wanajeshi Kipanga FC huku pia ikitamba kuimarika kimbinu baada ya kucheza na Simba kwenye Kombe la Muungano.

KVZ FC inashuka uwanjani leo kuwakabili Wanajeshi wa Kipanga FC katika mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri visiwani hapa.

KVZ FC ipo nafasi ya nne katika msimo wa Ligi ya Zanzibar yenye timu 16 hiyo ikiwa ni baada ya kujikusanyia point 37 kwenye michezo 20 iliyocheza

Akizungumza na gazeti hili jana Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Mohmed Ameir, alisema haangalii mchezo uliokuwa mbele yake dhidi ya Kipanga FC pekee bali michezo yote kumi iliyobakia.

Alisema katika michezo 10 hiyo wanataka kuhakikisha wanapata ushindi na kujikusanyia alama za mapema zitakazowafanya kutwaa ubigwa wa ligi hiyo.

Alisema kuelekea mchezo wao wa leo, tayari ameshazisoma mbinu nyingi za wapinzani wao na anajua zinapokutana timu hizo mchezo huwa mgumu, lakini kwa sasa amejiandaa kupata alama tatu.

"Tumejiandaa kurudi katika michezo ya ligi tukiwa na hamasa kubwa, michezo mitano ya mwisho kabla ligi kusimama hatukufanya vizuri sana, hivyo tumejipanga kuhakikisha mechi hizi zilizobaki tunafanya vizuri kwa kupata alama tatu ili kuweza kuzichanga vema karata zetu katika mbio za ubingwa," alisema.

Aidha, alisema kupitia mchezo mmoja ambao wamecheza dhidi ya Klabu ya Simba katika Ligi ya Muungano, umezidi kumpa mbinu mpya ambazo watazitumia kuwaangamiza wapinzani wao katika mchezo wa leo.

# *Malindi SC yashukuru sare kwa Mlandege FC*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa timu ya Malindi SC, Suleiman Mohmed 'Mo', amesema matokeo aliyoyapata ya alama moja dhidi ya Mlandege FC katika mchezo wao wa 'dabi' ya Zanzibar ndio aliyoyategemea kulingana na ugumu wa mchezo huo hasa kwa upande wao.

Malindi na Mlandege FC, juzi zilishindwa kutambiana baada ya kutoka sare isiyo na magoli katika mchezo wa mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar, ambao ulichezwa katika Uwanja wa Mau A visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kumalizika mchezo huo, alisema ingawa haikuwa lengo lake kupata matokeo hayo ya sare na aliamini zaidi kupata alama tatu, lakini hayakumuumiza.

Alisema wapinzani wao hao katika misimu hii miwili wapo katika kipindi cha kuboresha kikosi chao na pia hufanya vizuri katika mashindano mengine, hivyo alama moja aliyoipata kwake yeye ni bahati.

Mo alisema mchezo huo ulikuwa mgumu katika dakika zote 90 na kuzidiana mara nyingi, hivyo kupitia mechi hiyo ameona kikosi chake kimecheza vizuri ikilinganishwa na hapo awali.

"Matokeo haya ambayo tumeyapata si mabaya kulingana na hali ya kikosi chetu, lakini na timu tuliyocheza nayo, wapinzani wetu Mlandege FC wana wachezaji wazuri hivyo kuwadhibiti hadi tunagawana alama haikuwa kazi rahisi na ukiangalia mzunguko wa kwanza walitufunga mabao 2-0," alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Mlandege FC, Sabri China, alisikitishwa na timu yake kucheza chini ya kiwango na kushindwa kutumia vema nafasi nyingi walizozitengeneza.

Alisema bado anaendelea kutafakari tatizo lililowafanya wachezaji hao kutocheza vizuri katika mchezo huo muhimu kwao ili kuiondoa timu katika nafasi iliyopo.

Alisema hadhani kuwa kiwango walichoonesha wachezaji wake kinatokana na hofu ya mchezo huo wa dabi, kwa kuwa timu hizo zinajuana vizuri katika Ligi Kuu Zanzibar.

"Imenisikitisha sijui tatizo lilikuwa nini kwa hawa wachezaji, tumetengeneza nafasi nyingi za wazi lakini tumeshindwa kuzitumia, sisemi kama hawakuwa na umakini bali nadhani haikuwa bahati kwetu," alisema.

Kwa matokeo hayo timu zote zimefikisha alama 26 wakati Malindi SC ikiwa nafasi ya tisa Mlandege FC ipo nafasi ya 10.

Katika Uwanja wa Finya Kisiwani Pemba timu ya Chipukizi FC ilifanikiwa kuwadidimiza mkiani Maendeleo FC kwa kuwafunga mabao 2-0. Mabao yote ya Chipukizi yaliwekwa nyavuni na Faki Mwalimu katika dakika ya 57 na 68.

HABARI MICHEZO



# SILVA SASA ATHIBITISHA KUONDOKA CHELSEA

**LONDON.** England

THIAGO Silva amethibitisha kuondoka Chelsea mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Beki huyo mkongwe, ambaye alijiunga kwa uhamisho wa bure kutoka Paris Saint-Germain mwaka 2020, atafikisha umri wa miaka 40 Septemba na alitania uwezekano wa kuondoka Stamford Bridge mapema mwezi huu.

Akithibitisha uamuzi wake sasa wa kuondoka, Silva aliviambia vyombo vya habari vya Chelsea: "Chelsea ina maana kubwa kwangu. Nilikuja hapa kwa nia ya kukaa mwaka mmoja tu na ikaishia miaka minne. Si kwangu tu bali kwa familia yangu pia.

"Wanangu wanachezea Chelsea kwa hiyo ni fahari kubwa kuwa sehemu ya familia ya Chelsea - kwa sababu wanangu wapo hapa. Ninatumaini wanaweza kuendeleza maisha yao yapo hapa katika klabu hii ya ushindi ambayo wachezaji wengi wanatamani kuwa sehemu yake.

"Nadhani katika kila kitu nilichofanya hapa kwa miaka minne, nilijitolea kila wakati. Lakini, kwa bahati mbaya, kila kitu kina mwanzo, katikati na mwisho. Hiyo haimaanishi kuwa huu ni mwisho wa uhakika. Natamani kuondoka, mlango ufunguke ili siku za usoni nirudi, japo kwa nafasi nyingine hapa lakini ni upendo usioelezeka.

"Ni wazi, wakati naanza hapa, ilikuwa wakati wa janga kwa hiyo hakukuwa na mashabiki uwanjani. Lakini kupitia mitandao ya kijamii, ikawa kitu cha kipekee kwangu na ndipo mashabiki walipoanza kurudi uwanjani na maisha yakaendelea.

"Tayari ni vigumu kusema kwa heri katika hali ya kawaida, lakini kunapokuwa na upendo wa pande zote, ni ngumu zaidi."

# *Marc Guehi kwenye rada timu kubwa EPL*

**LONDON,** England



KLABU za Manchester United na Arsenal zote zina nia ya kumsajili beki wa kati wa Crystal Palace, Marc Guehi msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa The Times.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefurahia miaka mitatu ya kuvutia akiwa na Palace, lakini anakaribia miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake, kumaanisha huu ni msimu wa mwisho kwake na 'Eagles' wanaweza kutaka ada kubwa ili kumuuza.

Palace inahofia kwamba Guehi atataka kuondoka msimu huu wa majira ya joto, na wanajiandaa kudai ada ya rekodi ya klabu ya zaidi ya pauni milioni 55 ili kumuachia.

90min hapo awali iliripoti kuwa Guehi anatakiwa na Man United, Newcastle United, Tottenham Hotspur na Bayern Munich, huku Arsenal nayo ikijitosa kutafuta mbadala wa Jakub Kiwior, iwapo mchezaji huyo wa Kimataifa wa Poland ataondoka msimu huu wa majira ya joto.

Waajiri wa zamani Chelsea pia wamekuwa wakimfuatilia Guehi kwa miezi kadhaa na wana haki ya kufikia ofa yoyote ambayo Palace itakubali kumuuza mlinzi huyo.

United wanatarajiwa kuwa na mawasiliano na Palace msimu huu wa majira ya joto kwani pia wanataka kumnasa winga Michael Olise.

Inaeleweka kwamba, Mfaransa huyo ana nia ya kuhamia Old Trafford, ambako mmiliki mwenza mpya Sir Jim Ratcliffe anajulikana kumfuatilia Olise kwa miezi kadhaa.

Mkataba wa Olise unajumuisha kipengele tata cha kuruhusiwa kuondoka kwa thamani ya kati ya pauni milioni 50 na 60.

# Liver yaamua kuhusu Salah

**LIVERPOOL,** England



LIVERPOOL inatarajia Mohamed Salah kubaki katika klabu hiyo msimu ujao kwa mujibu wa The Athletic.

Salah anakaribia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake pale Anfield huku timu za Saudi Arabia zikiwa tayari kuweka dau kubwa la huduma yake na imependekezwa kuwa mwisho wa enzi ya Jurgen Klopp unaweza kuifanya Liverpool kupata fedha kwa Salah.

Tetesi za uwezekano wa kuondoka kwa Salah ziliongezeka mwishoni mwa wiki baada ya kubwatukiana hadharani na Klopp wakati wa sare ya mabao 2-2 na West Ham United, lakini The Athletic limeripoti kwamba Liverpool hawakubaliani na wazo la kumpoteza Salah.

Hakika, 'Wekundu' hao wanasemekana kupanga msimu ujao wakiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, kwenye kikosi chao, ambaye hajaonesha nia ya kuondoka Anfield kwa haraka.

Maofisa wa klabu pia wanasemekana kutamani Salah abakie, na hivyo kufanya kuondoka msimu huu wa majira ya joto kusiwe na uwezekano mkubwa, na ugomvi huo wa Jumamosi haujabadilisha chochote.

Wale wanaosimamia Ligi ya Saudia pia wanaamini nia ya sasa ya Salah ni kutumia angalau msimu mmoja zaidi Liverpool.

Mmisri huyo atapatikana kama mchezaji huru mkataba wake utakapokamilika Juni mwakani.

HABARI MICHEZO

## Yanga yachafua tena faili lake

INATOKA UKURASA 24

fanyia kazi madai ya Kambole ili kuweza kumalizana naye.

"Hili suala linamalizwa kiofisi, ni jambo ambalo tayari linafanyiwa kazi kuweza kulimaliza," alisema Kamwe.

TFF imezitaka klabu za soka nchini kuheshimu mikataba ambayo zimeingia na wachezaji pamoja na makocha ili kuepuka adhabu mbalimbali ikiwamo kufungiwa kusajili.

Kambole alijiunga na Yanga Juni 2022 akitokea Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, lakini Yanga waliamua kuachana naye msimu uliopita.

## Simba yaonywa mchakato mrithi wa Benchikha

INATOKA UKURASA 24

Makalla, ambaye kabla ya wadhifa huo mara ya mwisho, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, alisema hayo baada ya Klabu ya Simba kuvunja mkataba na kocha wake, Mualgeria Benchikha ambaye aliomba kufanya hivyo kwa kile alichodai kwenda kumuuguza mkewe.

"Ushauri wangu kwa Simba, sawa kocha ameondoka, sasa wakae, wahakikishe kocha wanampata haraka, siyo ameondoka viongozi wakafanya usajili wenyewe wakati haijapata mwalimu.

"Nashauri wampate kocha haraka, halafu huyo ndiye afanye usajili, isiwe kinyume chake, eti kocha hajapatikana halafu wanasajili, anakuja tayari wameshapata wachezaji wapya, hii haitokuwa sawa, matatizo yatakuwa ni yale yale," alisema Katibu huyo.

Kiongozi huyo pia aliitaka klabu ya Simba kutatua tatizo la msingi na si kukimbilia kuvunja mikataba wa makocha kama ambavyo imekuwa ikifanyika hivyo mara kwa mara pale timu inapokuwa haifanyi vizuri.

"Mimi huwa sipepesi maneno, Simba ni lazima itatue tatizo la msingi. Tuangalie Simba tatizo ni nini? Ni wachezaji? Je, ni uongozi? Ni makocha? Na kwa nini kila mara Simba ikitokea haifanyi vizuri ni kocha ndiye anafukuzwa au anaondoka? Sisi hatutakiwi kujitafakari kwamba tunawapa makocha wachezaji wanaotakiwa? Majukumu yetu kama viongozi tumeyatimiza? Nadhani imefika wakati tunaona kama vile pale Simba mgonjwa wa malaria anapewa dawa ya kupunguza maumivu, huwezi kupona ugonjwa ulionao," alisema Makalla.



# MGOSI AITAKA HESHIMA YA SIMBA QUEENS, BADO 7 TU

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

LICHA ya kubakiza pointi saba tu kabla ya kutangazwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara msimu wa 2023/24, Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema bado wana safari ngumu kuhakikisha wanaendelea kurejesha heshima ya klabu hiyo.

**Simba Queens juzi waliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya wapinzani wao wakuu, JKT Queens, katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.**

Yalikuwa ni mabao ya straika hatari wa timu hiyo, Aisha Mnuka na beki wa kati wa Kimataifa wa Kenya, Ruth Ingosi, yaliyoifanya timu hiyo, si tu kupata ushindi huo, lakini kufikisha jumla ya pointi 37, ambazo zinaifanya kuhitaji ushindi wa michezo miwili na sare moja katika michezo mitano iliyobaki ili kuweza kutwaa ubingwa huo.

Takwimu zinaonyesha kuwa iwapo Simba Queens itapata pointi saba, itafikisha jumla ya pointi 46 ambazo hazitafikiwa na timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu ya Wanawake inayoshirikisha timu 10.

Wakati timu zote zikiwa zimecheza mechi 13 na kubakisha mechi tano tu, Mabingwa Watetezi, JKT Queens baada ya kufungwa juzi wamebaki na pointi 28, ambazo kama ikishinda mechi tano zilizobaki itafikisha pointi 43, ambazo zitakuwa zimeshapitwa na Simba Queens, iwapo itashinda mechi mbili au tatu zijazo.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo juzi, Mgosi alisema pamoja na kuifunga JKT Queens, bado ligi inaendelea hivyo wanatakiwa kupambana kila mechi kusaka pointi tatu muhimu kufikia malengo yao yanayotarajiwa hususan kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Mgosi alisema mipango yao ni kuona wanafanikiwa kwenye malengo yao ikiwamo kurejesha heshima ya klabu hiyo hali ambayo inahitaji kushinda michezo iliyopo mbele yao. Aidha, aliwapongeza wachezaji wake kwa kufuata maelekezo na kuweza kupata ushindi na kurejesha heshima ya klabu hiyo kwa kumfunga JKT Queens.

"JKT Queens ni timu kubwa hapa nchini, kupata heshima Simba lazima uifunge timu kubwa kama JKT Queens, tumefanikiwa kumfunga mkubwa mwenzetu, lakini bado hatujachukua ubingwa ambayo ni malengo yetu.

"Kufikia malengo hayo ni lazima tupambane kushinda michezo iliyopo mbele yetu yote, kuifunga timu kubwa haina maana kuwa tupo bora zaidi kwa sababu tunaenda kukutana na timu zingine ambazo zimejipanga vizuri na unapokosea unaadhibiwa," alisema Mgosi.

Kocha wa JKT Queens, Ester Chabruma, alisema walijiandaa vizuri kwa mchezo huo na wamepoteza kwa makosa waliyoyafanya uwanjani ambayo yaliwafaidisha Simba kwa kupata ushindi.

"Kuhusu kutetea ubingwa wetu kwa sasa tuna mlima mrefu kutokana na Simba Queens kutuzidi alama tisa, lakini bado tutaendelea kupambana kwa sababu ligi bado haijaisha," alisema Chabruma.

Bingwa wa ligi hiyo, huiwakilisha nchi kwenye michuano ya CECAFA, ambayo pia hutumika na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kumpata mwakilishi wa Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa timu inayotwaa ubingwa huo.

Simba Queens na JKT Queens zimeiwakilisha Ukanda wa CECAFA mwaka juzi na uliopita zilipotwaa ubingwa na Afrika Mashariki na Kati.

MAGONGO...



Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Magongo ya TMK, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Serikali yaanika mkakati Stars kuwika Afcon 2027*

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Magomeni (CCM), Mwanakhamis Kassim Said, amehoji mikakati ya serikali ya kuihamasisha Timu ya Taifa (Taifa Stars), ili ifanye vizuri katika Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, kama inavyofanyika kwa Klabu za Simba na Yanga kwenye michuano ya kimataifa.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema ili mashindano hayo yafane nchini, lazima kuwe kuna timu inayoshiriki na kuhoji mkakati wa serikali wa kuisimamia timu ya taifa.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, alisema Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda zitakuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027.

"Ili kuhakikisha timu ya taifa inafanya vizuri katika mashindano hayo, serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwamo; ujenzi wa viwanja vya mpira katika majiji ya Dodoma na Arusha, ukarabati wa viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru pamoja na kuwatafuta na kuwaleta nchini wachezaji wenye asili ya Tanzania wanaoishi na kucheza nje ya nchi ili kuichezea timu ya taifa.

Alitaja mkakati mwingine kuwa ni kuwashirikisha wadau mbalimbali wa michezo kuchangia timu za taifa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha za kuzigharamia timu za taifa zinazoshiriki mashindano ya kimataifa.

Pia alisema kuwa uwenyeji wa mashindano ya CHAN mwaka 2024 ambayo ni maandalizi kwa timu ya taifa kuelekea AFCON 2027, kuajiri kocha na benchi la ufundi lenye sifa na uzoefu katika mpira wa miguu duniani na kuhudumia timu zote za taifa zinazoshiriki mashindano ya kimataifa.

Michezo

Jumatano Mei 1 2024

Nipashe



Liver yaamua kuhusu Salah UKURASA 22

KAZI IMEANZA...




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (kulia), akimkabidhi mkataba winga mpya wa timu hiyo, Frank Tiesse, kutoka Klabu ya Stade Malien ya Mali, baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo kuanzia msimu ujao. Pembeni anayeshuhudia ni wakala wa mchezaji huyo. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Simba yaonywa mchakato mrithi kocha Benchikha

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

## Washauriwa kufanya haraka huku viongozi wakitakiwa kujitathimini kwa...

WAKATI Klabu ya Simba ikieleza tayari imeanza mchakato wa kumsaka kocha mpya wa kurithi mikoba ya Abdelhak Benchikha aliyeachana na timu hiyo mwishoni mwa wiki, viongozi wa klabu hiyo wameonywa na kutakiwa kujitathimini kwanza.

**Benchikha na Simba walifikia makubaliano ya pande zote za kuvunja mkataba baada ya kocha huyo kuhudumu chini ya msimu mmoja.**

Akizungumza na Nipashe jana kutoka Ruangwa mkoani Lindi, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema tayari viongozi wameanza kusaka kocha mpya kutokana na vigezo walivyoviweka.

"Nipo nje ya ofisi, lakini kwa uhakika tayari viongozi wameanza mchakato wa kusaka kocha wetu mpya, taratibu zipo hatua ya awali na mambo yakienda sawa mashabiki na wanachama wetu wataambiwa kila kitu," alisema Ahmed.

Alisema viongozi wapo kwenye mchakato huo na wapo makini kuhakikisha wanapata kocha mwenye uwezo mkubwa na sifa za kuifundisha timu hiyo.

"Lazima atakuwa kocha mwenye viwango vikubwa, Simba ni timu kubwa, hivyo lazima ipate kocha anayeendana nayo... mchakato huu wa kumpata kocha mpya unafanywa kwa weledi mkubwa," alisema Ahmed.

Jana, Juma Mgunda, aliiongoza Simba kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Namungo FC kama kocha mkuu wa muda akichukua nafasi ya Benchikha.

Wakati huo huo Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amewataka viongozi wa Simba kufanya haraka mchakato wa kumpata kocha mpya ili ahusike na usajili wa wachezaji wa msimu ujao, badala ya kufanya usajili wenyewe na kumleta kocha baadaye kama ambavyo wamekuwa wakifanya kwa misimu ya karibuni.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Makalla, ambaye ni shabiki na mwanachama wa klabu hiyo, pia amewataka viongozi wa klabu hiyo kujitathimini kwani imekuwa ni kawaida kwa klabu hiyo makocha kuondoka au kutimuliwa baada ya timu kufanya vibaya, akisema inabidi sasa kitafutwe chanzo cha matatizo yote hayo, badala ya kuwaangushia jumba bovu walimu.

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yachafua tena faili lake FIFA

**Na Faustine Feliciane**

IKIWA ni siku chache tu tangu ifungiwe na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), kufanya usajili kutokana na kukiuka kanuni za uhamisho, Klabu ya Yanga imechafua tena faili lake katika shirikisho hilo baada ya kuzuiwa kwa mara ya pili kusajili kutokana na kosa lingine tofauti na lile la awali.

Aprili 12, mwaka huu, TFF ilitoa taarifa kwa umma kuwa FIFA imeifungia Yanga kusajili kutokana na kukiuka kanuni ya uhamisho za kile kilichoitwa Annexe 3 ya Kanuni ya Uhamisho (RSTP) ya shirikisho hilo.

Taarifa hiyo ikieleza kuwa Yanga haikuingiza uthibitisho wa malipo wa uhamisho wa mchezaji husika (ambaye haikumtaja) katika usajili (TMS), licha ya kukumbushwa kufanya hivyo mara kwa mara na kwamba suala hilo lipo mezani kwa Sekretarieti ya Nidhani ya FIFA kwa hatua zaidi.

Hata hivyo, wakati suala hilo likiwa bado la moto na wadau wa soka wakisikilizia kile ambacho Sekretarieti ya Nidhani ya FIFA, itaamua mbali na adhabu hiyo ya kufungiwa, jana TFF ilipokea taarifa kutoka shirikisho hilo la soka duniani na kuitoa kwa umma kuwa Yanga imefungiwa tena kusajili kutokana na kutolipa malimbikizo ya mishahara pamoja na fidia ya kuvunja mkataba na aliyekuwa mchezaji wao, Mzambia Lazarus Kambole.

Kwa mujibu wa taarifa ya TFF, mchezaji huyo raia wa Zambia alifungua kesi FIFA kuitaka Yanga kumlipa malimbikizo ya mishahara yake pamoja na fedha za fidia za kuvunjiwa mkataba wake na klabu hiyo.

TFF ilienda mbali zaidi na kuweka wazi na wao wameifungia Yanga kusajili wachezaji wa ndani mpaka pale watakapomlipa nyota huyo.

Hata hivyo, akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Msemaji wa klabu hiyo, Ally Kamwe, alisema uongozi wa klabu hiyo una-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002